SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la
# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 38, Septemba 2024

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha



# TRC YANYAKUA TUZO KWA UBORA WA KUHABARISHA UMMA

**Na Mwandishi wetu.**



Shirika la Reli Tanzania - TRC kupitia kitengo cha Habari na Uhusiano kwa Umma imeibuka kidedea kwa kunyakua tuzo ya Uandishi Wenye Tija (Stories of Change) za mwaka 2024 zinazotolewa na taasisi ya Jamii Forums na kuwa taasisi ya Serikali inayohabarisha umma kwa usahihi na wakati, Septemba 2024.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma Bi. Jamila Mbarouk ameeleza kuwa tuzo hizo ni za kipekee kwa kuwa wananchi wameweza kupiga kura na kuichagua TRC kuwa taasisi ya Serikali inayofanya vizuri katika kuhabarisha umma kwa wakati.

“Jukwaa lililoweza kuchagua kazi za TRC ni jukwaa huru, wananchi wameona ufanisi wa kazi za TRC na kushirikiana nao pindi wanapohitaji ufafanuzi wa taarifa” alisema Bi. Jamila.

Inaendelea Uk. 2

# TRC YANYAKUA TUZO KWA UBORA WA KUHABARISHA UMMA

Inatoka Uk. 01

Bi. Jamila alisema kuwa tuzo hiyo itaendelea kuleta tija kwa Shirika la Reli Tanzania kwa kuwa wananchi wanaona kazi nzuri zinazofanywa na TRC na kuwahakikishia TRC itaendelea kushirikiana na umma katika kuwapa taarifa kwa usahihi na wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya Jamii Forums Bw. Mexence Melo alisema kuwa pasi na kuwa na malalamiko yaliyojitokeza kabla na baada ya uendeshaji wa mradi wa SG, TRC imekua ya kipekee kwa kutoa majibu kwa wananchi na kuchukua hatua kwa wakati.

“TRC ni miongoni mwa taasisi za mfano wamekua wakichua hatua pale yanapotokea masuala ambayo wananchi wanahitaji yafanyiwe kazi” alieleza Bw. Melo.

Shirika la Reli Tanzania limepewa dhamana na Serikali kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujenga reli yenye kiwango cha kimataifa na hivi sasa TRC imeanza kutoa huduma za reli hiyo kwa kutumia treni za kisasa zenye kutumia nishati ya umeme.






Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi. Jamila Mbarouk (kushoto) akizungumza na Mkurugenzi wa Jamii Forums Bwana Maxence Melo mara baada ya kupokea Tuzo ya **"Stories of Change"** katika kipengele cha Taasisi ya Serikali inayohabarisha umma kwa usahihi na wakati kwa mwaka 2024 katika Hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam Septemba 21, 2024.

# SGR NA MABADILIKO KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI



**Na Mwandishi wetu.**

Ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ulianza tarehe 12 Aprili, 2017 chini ya uongozi wa awamu ya tano ya Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Ujenzi wa SGR nchini Tanzania kama ujenzi mwingine wowote mkubwa wa reli barani Afrika ni miongoni mwa Mtandao wa Reli ya Kasi ya Juu barani Afrika (AIHSRN) yenye kasi ya 160km kwa saa kwa treni za abiria na 120km kwa saa kwa treni za mizigo ambao unalenga kuunganisha nchi 16 za Afrika zisizo na bandari kupitia bandari za bahari na maziwa makuu na kuunganisha nchi mbalimbali kwa kuanzisha kanda za usafirishaji na kuunganisha miundombinu ya usafirishaji katika njia muhimu za usafiri na kuunganisha miji mikuu ya kisiasa na kiuchumi.

Ujenzi wa SGR Tanzania unajengwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi imegawanyika katika sehemu tano, kipande cha kwanza cha ujenzi Dar es Salaam - Morogoro chenye urefu wa kilomita 300, kipande cha pili cha ujenzi ni Morogoro - Makutupora chenye urefu wa kilomita 426, kipande cha tatu kinaanzia Makutupora – Tabora kina urefu wa kilometa 368, kipande cha nne cha ujenzi ni kutoka Tabora – Isaka chenye urefu wa kilomita 130 na kipande cha tano kutoka Mwanza - Isaka chenye kilomita 341, wakati huo huo ujenzi wa awamu ya pili wa SGR umeanza kutoka Tabora – Kigoma chenye urefu wa kilomita 506.

Hata hivyo, matarajio ya baadaye ya Serikali ni kuongeza ujenzi wa mtandao wa SGR kuendelea kuunganisha taifa, watu na rasilimali pia kuunganisha Tanzania na nchi za jirani ili kuzitumia fursa zilizopo katika nafasi ya Tanzania kijiografia.

Akielezea mipango ya TRC, Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu kutoka Shirika la Reli Tanzania Mhandisi Machibya Masanja amesema kuwa ujenzi wa SGR utapita hadi Isaka - Rusumo urefu wa kilomita 371 na kuwa sehemu ya reli ya SGR ya Isaka – Kigali.

Aidha, Mhandisi Machibya alieleza kuwa Januari,

**Inaendelea Uk. 04**

# SGR NA MABADILIKO KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

Inatoka Uk. 03

2022 Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini Mkataba wa Makubaliano ya ujenzi wa reli ya SGR inayounganisha nchi hizo mbili kupitia sehemu ya Uvinza – Malagarasi ambayo itakuwa sehemu ya reli ya Tanzania na Burundi ambapo kipande chenye urefu wa Kilometa 180 za reli zitaanzia Uvinza – Tabora - Kigoma hadi mto Malagarasi kwenye mpaka wa Burundi na sehemu ya kilomita 187 itajengwa kuunganisha mji wa mpaka wa Musongati na mji mkuu Gitega.

Kukamilika kwa mtandao wa SGR kutaunganisha reli ya Kusini mwa Tanzania ya Mtwara - Mbamba Bay ambayo inapanua wigo kwa bahari ya Hindi hadi ziwa Nyasa itakayopita mikoa yenye madini ya chuma, makaa ya mawe na grafiti. Pia itahudumia migodi ya makaa ya mawe na chuma ya Mchuchuma na Liganga.

Ili kuhakikisha shughuli za uendeshaji zinaendelea baada ya kukamilika kwa ujenzi wa SGR ambapo shughuli za awali za uendeshaji zimeanza tangu tarehe 14 Juni, 2024 kwa treni za Dar es Salaam – Morogoro na baadaye Julai 25, 2024 kwa treni za Dar es Salaam – Dodoma, Serikali kupitia TRC imenunua vifaa mbalimbali vya uendeshaji.

Ununuzi mkubwa wa vifaa kwaajili ya reli ya kiwango cha kimataifa umegawanyika katika makundi sita (6) ambapo kundi la kwanza linahusisha ununuzi wa injini za dizeli, kundi la pili ni ununuzi wa treni za umeme, kundi la tatu ni ununuzi wa treni za abiria za vichwa mchongoko 'Electric Multiple Unit (EMU), kundi la nne ni ununuzi wa mabehewa ya abiria ya ghorofa , kundi la tano ni ununuzi wa mabehewa ya mizigo na kundi la sita ni ununuzi wa vifaa na mashine za matengenezo ya njia.

Shirika la Reli Tanzania limekuwa likinunua vifaa vya uendeshaji kutoka makampuni mbalimbali ambapo vichwa vya treni 17 vya SGR vinavyotumia nishati ya umeme vilinunuliwa kwa mkataba kati ya TRC na Hyundai Rotem ya Korea Kusini na vyote vimewasili nchini tayari kwa kazi na majaribio mengine ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji kazi. Hata hivyo, seti kumi (10) za treni za vichwa mchongoko 'Electrical Multiple Unit' (EMU) zilinunuliwa katika mkataba kati ya TRC na Hyundai Rotem kampuni ya Korea Kusini, Seti tatu (3) zimepokelewa na TRC na ziko katika hatua za mwisho za majaribio kabla ya kuanza kazi,

Aidha, mabehewa thelathini (30) ya ghorofa yalinunuliwa kutoka kampuni ya Leuckemeia ya Ujerumani na kati yao mabehewa sita (6) yamepokelewa na TRC na mwisho mabehewa ya abiria Hamsini na Tisa (59) yalinunuliwa kutoka Kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology (SSRST) ya Korea Kusini na mabehewa yote yamepokelewa na TRC na yanafanya kazi katika uendeshaji wa treni za SGR Dar es Salaam- Morogoro – Dodoma.

Kusimamia ukuaji wa baadaye wa usafirishaji wa reli katika ukanda huu, usafirishaji wa mizigo utakuwa biashara kuu tarajiwa katika kuhakikisha ukuaji wa biashara na viwanda nchini na kuunganisha Tanzania na nchi nyingine za ukanda wa Afrika

Inaendelea uk. 05



# SGR NA MABADILIKO KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

Inatoka Uk. 4

Mashariki na kati, hivyo Serikali imenunua mabehewa 1,430 yatakayotumika wakati wa shughuli za uendeshaji.

Ushirikiano uliopo kati ya TRC na wadau mbalimbali utaiwezesha TRC kupata mapato kwa njia ya uwekezaji wa wazi (Open Access) ambapo sekta binafsi itakuwa na uwezo wa kuwekeza kwa kununua mabehewa yao wenyewe na kulipia tozo ya njia (accessibility) hii itahakikisha upatikanaji wa kutosha wa mabehewa na kuongeza ushindani kati ya wafanyabiashara pamoja na kuhakikisha uharaka katika usafirishaji hivyo itapelekea Serikali kupata mapato kubwa kwa kusafirisha mizigo.

Lengo la uwekezaji wa wazi katika uendeshaji wa SGR utawezesha Serikali kuhudumia shehena nyingi ikiwa ni pamoja na kuongeza ufanisi na ushindani utakaomuwezesha mwananchi kupata huduma ya uhakika na bora zaidi. Serikali ya Tanzania imewekeza katika ujenzi wa bandari kavu na treni za mizigo jambo linalovutia ukuaji wa Biashara na Viwanda.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa kwenye mahojiano na waandishi wa habari alisema kuwa lengo la SGR ni kuanzisha njia ya kimataifa inayounganisha Tanzania na nchi jirani na bandari ya Mashariki ya jiji la Dar es Salaam kupitia reli kwa gharama nafuu kulinganisha na usafiri wa barabara.




Moja ya treni za mwendokasi zilizonunuliwa na Serikali ya Jmahuri ya Mungano wa Tanzania ikiwa katika stesheni ya Dar es Salaam kwaajili ya kutoa huduma ya usafiri wa abiria.

Kwa maelezo ya kina zaidi SGR inakusudiwa kupunguza msongamano barabarani ambapo kila treni ya mizigo inatarajiwa kusafirisha hadi tani 10,000 za mizigo sawa na malori 500 barabarani. Zaidi ya yote, ujenzi na uendeshaji wa SGR umechochea upatikanaji ajira, hii ni pamoja na kazi za ujenzi, matengenezo, uendeshaji na katika viwanda vinavyonufaika na uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji.

Uendeshaji wa treni za SGR kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Morogoro unaendelea na TRC inakabiliwa na ongezeko kubwa la abiria wanaosafiri na treni za SGR ambapo kuanzia Juni 14, 2024 hadi Agosti 30, 2024 TRC imesafirisha abiria 412,449.



Moja ya treni za mwendokasi zinazotumia nishati ya umeme (Electric Multiple Unit - EMU) ikiwa katika majaribio kabla ya kuanza kutoa huduma hivi karibuni.



Sehemu ya miundombinu ya reli iliyopo eneo la kituo cha kupangia treni za mizigo (Marshalling Yard) lililopo Kwala mkoani Pwani.

# UWEPO WA SGR UNAASHIRIA UTOSHELEVU WA UMEME NCHINI - DKT. BITEKO



**Na Mwandishi wetu.**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko amesafiri na treni ya mwendokasi (SGR) kwa mara ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma Septemba 12, 2024.

Dkt. Biteko amesema safari za treni za SGR zinazotumia umeme kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ni ushahidi kuwa Tanzania ina umeme wa kutosha.

"Safari za treni ya umeme ya SGR ni ushahidi mwingine kuwa nchi ya Tanzania ina umeme wa kutosha, ni ushahidi mwingine kwamba nishati ya umeme ikipatikana ya uhakika inafungua fursa mbalimbali za kiuchumi, viwanda mbalimbali vinajengwa na kongani za viwanda kuongezeka," alisema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa katika kuhakikisha umeme unatosheleza, Wizara ya Nishati kazi yake ni kuhakikisha umeme unakuwepo wa kutosha wakati wote na kuwa Wizara inasimamia ujenzi wa njia nyingine ya kutoa umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma kwa laini kubwa zaidi na kutoa umeme kutoka Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere kwenda Dodoma baadae Singida, Arusha hadi Mwanza.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko akizungumza na baadhi ya abiria ndani ya treni ya mwendokasi (SGR) alipokuwa safarini kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma Septemba 12, 2024.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Mwanza mara baada ya ujenzi kukamilika.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Isaka mara baada ya ujenzi kukamilika.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Malampaka mara baada ya ujenzi kukamilika.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Fela mara baada ya ujenzi kukamilika.



Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Shinyanga mara baada ya ujenzi kukamilika.




Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR ya Tabora mara baada ya ujenzi kukamilika.

# HUDUMA ZA USAFIRI WA TRENI YA SGR

Usafiri wa treni katika reli yenye kiwango cha kimataifa (SGR) ni moja kati ya usafiri wa haraka na nafuu uliowahi kutokea nchini Tanzania. Reli hii ya SGR ya nchini Tanzania hadi sasa ndio reli pekee inayotumia nishati ya umeme Afrika Mashariki ikijumuisha nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na Congo.

Mbali na kusafiri, zipo huduma na taratibu mbalimbali zinazotolewa kabla na baada pindi unapotaka kusafiri na treni inayotumia nishati ya umeme.






## UKATAJI TIKETI

Ukataji wa tiketi ambao ni hatua ya mwanzo pindi abiria anapohitaji kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, abiria anaweza kukata tiketi kupitia madirisha ya kukatia tiketi ndani ya stesheni au kupitia mfumo wa sgrticket.trc.co.tz. Kupitia mfumo abiria anaweza kuchagua mji anaotoka na mjini anaokwenda, kisha atachagua tarehe ya safari, atajisajili, baada ya hapo abiria atachagua namba ya behewa na siti kisha atapata nauli na baadaye namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali.

Malipo hufanyika katika njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya simu, benki, wakala wa benki au katika stesheni iliyo karibu kwa huduma zaidi.

## VITAMBULISHO

Yapo mambo muhimu ambayo abiria anatakiwa kuzingatia kama kuwa na kitambulisho (uraia, leseni ya udereva, hati ya kusafiria, kitambulisho cha kazi) endapo abiria hatokuwa na kitambulisho anapaswa kuwa na barua ya Serikali ya mtaa yenye muhuri na picha. Kwa mtoto mwenye umri wa miaka minne hadi kumi na miwili anatakiwa awe na nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha shule, hati ya kusafiria au bima ya afya.

Uzito wa begi unaoruhusiwa kwa daraja la uchumi ni kilogramu 20 na daraja la biashara ni kilogramu 30 ambapo kipimo cha begi kisizidi urefu wa 72cm na upana wa 40cm na kimo cha 30cm.



# HUDUMA ZA USAFIRI WA TRENI YA SGR



### VITU VISIVYORUHUSIWA


Baadhi ya vitu kama mifuko ya plastiki, ndoo/ jaba, chakula, vinywaji, shangazi kaja, viroba, silaha, vilipuzi, vifaa vya mazoezi, betri zenye asidi zinazoweza kuvuja, vitu haramu, dawa za kulevya pamoja na wanyama hivyo vyote havitaruhusiwa kwa abiria kusafiri navyo kwakuwa vinahatarisha usalama na mazingira ndani ya treni.

Maswali ni mengi kutoka sehemu mbalimbali juu ya kuahirisha ama kubadilisha safari, abiria anatakiwa kuingia kwenye mfumo sgrticket.trc.co.tz kisha atabofya chagua tiketi, weka namba ya tiketi ama kumbukumbu namba ya malipo, weka pendekezo la tiketi ya safari, kuchagua behewa na siti, kisha abiria atafanya malipo na kuchapisha tiketi.

### KUAHIRISHA AU KUBADILISHA SAFARI

Kuahirisha ama kubadilisha safari, abiria anatakiwa kuingia kwenye mfumo sgrticket.trc.co.tz kisha atabofya chagua tiketi, weka namba ya tiketi ama kumbukumbu namba ya malipo, weka pendekezo la tiketi ya safari, kuchagua behewa na siti, kisha abiria atafanya malipo na kuchapisha tiketi.

Endapo abiria atahitaji kuahirisha safari na kurejeshewa fedha, abiria anapaswa kuandika barua ya madai kwenda kwa mkurugenzi mkuu pamoja na kuambatanisha tiketi husika, barua hiyo itumwe masaa matatu kabla ya muda wa safari.




### HUDUMA YA KUHIFADHI MIZIGO

Unaweza kuhifadhi mizigo katika stesheni kwa kutembelea dirisha la uhifadhi mizigo ukiwa na Kitambulisho na tiketi, lipia gharama za kuhifadhi mzigo kisha hifadhi mzigo kwa muda uliolipiwa. Endapo abiria atapoteza vitu atatakiwa kutoa taarifa kuhusu vitu vilivyopotea katika dirisha la uhifadhi mizigo au dirisha la vitu vilivyopotea. Vitu vilivyopatikana venye asili yakuoza vitahifadhiwa kwa siku 3 kabla ya kuteketezwa na vitu vilivyopatikana visivvooza vitahifadhiwa kwa siku 90 kabla ya kuteketezwa.

Orodha ya vitu visivyochukuliwa itachapishwa kwenye bango la Stesheni au chanzo kingine cha taarifa. Vitu ambavyo vitabainika kuwa na hatari kama vile vilipuzi, vifaa vinavyoweza kuwaka, sumu na kuambukiza, mionzi, na vinavyoweza kuyeyuka vitaripotiwa kwa mamlaka husika.

# MAHAFALI YA 30 YAFANA SHULE YA MSINGI ITIGI RELI



Bi. Amina Lumuli, Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC akizungumza wakati wa mahafali ya 30 ya Shule ya Itigi Reli mkoani Singida, Septemba 2024.



Bi. Amina Lumuli, Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC akimkabidhi zawadi Mwanafunzi Anna Cosmas wakati wa mahafali ya 30 ya Shule ya Itigi Reli mkoani Singida, Septemba 2024.

**Na Mwandishi wetu.**

Mahafali ya 30 ya Shule ya Msingi Itigi Reli kwa Wahitimu wa darasa la saba yamefanyika mkoani Singida, Septemba 2024.

Shirika la Reli Tanzania - TRC lilianzisha shule ya Itigi Reli ikiwa na lengo la kurahisisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wa wafanyakazi wa reli ambao walikuwa wakifanya kazi ya kulinda na kutunza miundombinu ya reli. Mgeni rasmi katika mahafalai ya 30 ya Shule ya Itigi Reli alikuwa Bi. Amina Lumuli, Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala TRC ambaye alieleza kuwa umuhimu Shule ya bweni Itigi Reli tangu kuanzishwa kwake 1987 ni kuhakikisha watoto wa wafanyakazi wanapata huduma zote muhimu zinazohusiana na masomo.

Shule ya bweni ya Itigi imekuwa ikifanya vizuri katika Mitihani yake ya ndani na nje, katika wilaya ya Itigi na mkoa wa Singida kwa ujumla ikishika nafasi ya kwanza hadi ya tatu kwa miaka mitatu mfululizo kwa mwaka 2021, 2022, 2023 huku wanafunzi wakifaulu kwa asilimia 100.

Shule imekuwa ikifanya vizuri kwa miaka mitatu mfululizo huku ikichagizwa na ushirikiano uliopo baina ya watumishi wa shule kwa kuwajibika kwa utaratibu ulipangwa kwa vitengo, mathalani walezi wakifanya kazi yao vizuri, wapishi kupika kwa wakati, hii inapelekea urahisi kwa. walimu kutoa taaluma darasani

“Watoto wana utayari, kila mmoja anatamani kumshinda mwenzake, nguvu waliyowekeza waendelee kuziishi ili kuendelea kufanya vizuri Sekondari” Grace Gyunda Mwalimu Mkuu wa Itigi Reli alisema

Mwanafunzi Jacob Petro amesema kuwa katika Mtihani waliofanya wa kumaliza Shule ya Msingi darasa zima litafaulu na wengine kwenda shule za vipaji kutokana na kujitoa kwa juhudi katika masomo darasani.

Mzazi Bi. Catherine Hajji amewaasa wanafunzi waliomaliza katika Shule ya Bweni Itigi Reli kuendelea kuyaishi mafunzo bora na mema waliyofundishwa na kuelekezwa na walezi wao shuleni mara watapokuwa katika mazingira ya nyumbani.

Shirika limedhamiria kufanya maboresho makubwa ya mazingira ya shule, kuchukua watoto wa wafanyakazi wengine walioko katika mazingira tofauti na kuhudumia wananchi wa Itigi kwa kuwa uhitaji wa huduma ya elimu umekuwa mkubwa.



**BODI YA WAHARIRI**
**MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary**
**HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy**
**PICHA | Hassan Mbonde, Augustino Bulegea**